



JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA
OFISI YA RAIS, UTUMISHI NA UTAWALA BORA
WAKALA YA SERIKALI MTANDAO

Samora, Avenue, ExTelecoms House, 2nd Floor, P.O Box 4273, Dar es Salaam, Tel: +255222129868/74, Fax: +255222129878,
General eMail: info@ega.go.tz, CEO eMail: ceo@ega.go.tz, Website: www.ega.go.tz



TAARIFA KWA VYOMBO VYA HABARI.

Serikali inaziagiza taasisi zote za umma kuhuisha taarifa katika tovuti zake, Tovuti Kuu ya Serikali (www.tanzania.go.tz) na kupokea na kujibu hoja za wananchi katika Tovuti ya Wananchi (www.wananchi.go.tz) ili kuwapatia wananchi huduma bora.

Tangu kuanzishwa kwa tovuti hizo kumeongeza kasi ya utendaji, uwazi, ufanisi, uwajibikaji na tija katika utoaji wa taarifa na huduma kwa wananchi. Hata hivyo, tathmini iliyofanywa na Wakala ya Serikali Mtandao ikishirikiana na Idara ya Habari-MAELEZO imeonesha changamoto kadhaa katika usimamizi wa tovuti hizo.

Changamoto hizo ni baadhi ya tovuti za taasisi za umma kutokuwa na taarifa mpya na za mara kwa mara, na kutofuatwa mwongozo iliyowekwa unaosisitiza usanifu wa tovuti hizo.

Hali hiyo imesababisha uwepo wa tovuti zisizokidhi viwango na ubora kufuatana na mahitaji ya watumiaji, gharama kubwa za uendeshaji, taarifa zilizopitwa na wakati, kutopatikana mara kwa mara, kukosa mifumo ya usalama ya kuzilinda na pia idadi kubwa ya tovuti hizo kuwa katika zama za kutoa taarifa tu na sio huduma.

Hivyo, katika kutatua changamoto hizo, maafisa mawasiliano na wataalamu wa TEHAMA wanaagizwa kuanza mara moja kuhuisha tovuti hizo na pia kuhuisha taarifa zao kwenye tovuti kuu zilizotajwa hapo juu na mwisho wa mwezi huu taasisi zitakazoshindwa kutekeleza zitaanikwa hadharani na hatua nyingine za kiutawala kuchukuliwa.

Serikali pia ili kuzisaidia taasisi hizo imeandaa Mwongozo unaolenga kutoa utaratibu wa kufuatwa na kuzingatwa katika Kusimamia na Kuendesha Tovuti za Serikali wa mwaka 2014.

Mwongozo huo unalenga kutatua changamoto hizo na kuziwezesha taasisi za umma kuandaa tovuti zenye mwonekano unaoshabihiana, utakaokidhi mahitaji ya wadau na pia kuwapa urahisi wa kuvinjari wakati wa kutafuta taarifa au kupata huduma kupitia tovuti hizo, kutoa maelekezo ya kuongeza ubora na usalama wa tovuti za Taasisi za umma na kutoa uelewa wa kutosha kwa mtumiaji kuhusu taarifa na huduma za Serikali.

